# EDU SERIES EXAM

## KISWAHILI STD 6

# KISWAHILI DARASA LA 6

**Muda:** Saa : 1 Dakika 40

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi emepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.**


Nilifika nyumbani na kupata maji _1_ ndani ya sufuria _2_ juu ya meko _3_ kupika chai _4_ mtoto. Mtoto huyo alikuwa akilia _5_ ya njaa. _6_ ya chai kuiva, mama alimwaga _7_ kikombe. Mtoto alifurahia sana kunywa chai. Pia mama _8_ mayai mawili na _9_. Mtoto alishiba ndil. Alitoka na kwenda kucheza na marafiki _10_. Walicheza kandakanda kwa _11_ mrefu sana. Walipochoka, walikaa chini na kupumzika. Watoto wote walitiririkwa na jasho kwenye miili yao. Walipumzika kwa _12_ halafu wakaanza kucheza mchezo wa kujificha na kutafutana, yaani _13_. Wakati wa _14_ watoto wote walienda nyumbani kula chamcha. Siku hiyo _15_ ya furaha kwa watoto hao.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. yakiwa | B. ukiwa | C. ikiwa | D. zikiwa |
| 2. | A. yaliwekwa | B. kiliwekwa | C. iliwekwa | D. liliwekwa |
| 3. | A. iyo | B. ili | C. ila | D. ile |
| 4. | A. za | B. cha | C. ya | D. vya |
| 5. | A. kwa sababu | B. lakini | C. kwasababu | D. wala |
| 6. | A. Bila | B. Badala | C. Kabla | D. Baada |
| 7. | A. ndani mwa | B. kwa | C. katikati | D. ndani ya |
| 8. | A. alimkarangia | B. alimkaangia | C. alimkaanga | D. alimkorogea |
| 9. | A. kumpea | B. kumpa | C. kumchukua | D. kumtoa |
| 10. | A. zake | B. wake | C. yake | D. mwake |
| 11. | A. muda | B. siku | C. mda | D. wiki |
| 12. | A. lisaa moja | B. saa moja | C. lisa limoja | D. saa limoja |
| 13. | A. jugwe | B. kwata | C. kibemasa | D. riadha |
| 14. | A. asubuhi | B. jioni | C. alasiri | D. adhuhuri |
| 15. | A. ilikuwa | B. ulikuwa | C. itakuwa | D. utakuwa |

**Kwa nambari 16 mpaka 30 jibu kulingana na maagazo uliyopewa**.

16. Ni kipi si kivumishi cha pekee?
    A. Wote B. Nzuri
    C. Jingine D. Chenyewe.
17. Utamwitaje mtoto wa mjomba?
    A. Shangazi B. Shemeji
    C. Ami D. Binamu
18. Anayewakilisha nchi yetu huko Uganda kwa niaba ya Raisi ni
    A. Diwani B. Jasusi
    C. Balozi D. Yahe
19. Andika wingi wa sentensi ifuatayo.
    Mtume amebeba barua mkononi
    A. Watume wamebeba barua mikononi
    B. Matume wamebeba barua mikononi
    C. Mitume wamebeba barua mikononi
    D. Tume zimebeba barua mikononi.

20. Umbo hili ni?



A. Pembe tatu duara
B. Pembe tatu mraba
C. Pembe tatu pacha
D. Pembe tatu sawa

21. Kanusha sentensi hii:
Kuchelewa kwake kulifaa.

A. Kulichelewa kwake hakukufaa
B. Kutochelewa kwake hakukufaa
C. Kutochelewa kwake hulifaa
D. Kuchelewa kwake hakukufaa

22. Alfajiri pia ni _

A. Macheo
B. Machweo
C. Adhuhuri
D. Jioni

23. Andika kwa wakati timilifu
Yeye alikuja kwa haraka

A. Yeye hajaja kwa haraka
B. Yeye amekuja polepole
C. Yeye amekuja kwa haraka
D. Yeye anakuja kwa haraka

24. Akisami ⅔ huitwaje?

A. thumuni mbili
B. nusu tatu
C. thuluthi mbili
D. humusi mbili

25. kitenzi kimbia katika kauli ya kutendesha ni

A. Kimbiwa
B. Kimbisha
C. Kimbiza
D. Kimbiwa

26. Neno mbao liko katika ngeli ya

AI–ZI B.U–ZI
C.I–I D. Li – Ya

27. Kinyume cha funika ni?

A. Fungua B. Funua
C. Funika D. Funisha

28. Ukubwa wa neno msitu ni ___

A. Kisitu B. msitu
C. misitu D. situ

29. Andika kwa
maneno. Watoto 13.

A. Watoto kumi na watatu.
B. Watoto kumi na tatu .
C. Watoto wakumi na tatu.
D. Watoto wakumi na watatu.

30. Tumia “amba” kukamilisha sentensi ifuatayo.
Kipepeo _____ ameruka ni huyu.

A. Ambacho B. Ambao
C. Ambalo D. Ambaye.

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.</u>**

Usafiri ni sehemu muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku. Tuna usafiri mbalimbali kama vile wa angani, majini na barabarani. Usafiri ambao hutumika sana ni ule wa barabarani ambapo watu hutumia baiskeli, magari, pikipiki, tuktuk, riksho na kadhalika. Kuna magari ya kibinafsi na yale ambayo si ya kibinafsi. Magari ambayo si ya kibinafsi humlazimisha mtumiaji kulipa nauli.

Usafiri ambao humlazimu mtu kutumia pesa nyingi sana ni ule wa angani. Usafiri huo wa angani humhitaji mtu aianze safari yake na kukamilisha katika uwanja wa ndege au angatua. Usafiri wa aina hii pia ndio wa haraka sana. Mara nyingi hutumiwa na watu wasiotaka kupoteza wakati au iwapo vifaa vinavyosafirishwa vinaweza kuharibika.

Njia ya usafiri ambayo huwaangamiza watu sana ni ile ya barabarani. Ajali za barabarani hufanya watu wengi wafariki. Kila mara utasikia kuwa gari limeanguka, magari yamegongana au hata gari limemgonga mtu. Sababu kuu ya ajali za barabarani ni kutojali kuwa watu wanaotumia barabara. Wengi hawafuati maagizo na sharia za barabarani.

Ni mara ngapi wewe umesafiri ndani ya gari bila kuufunga mshipi au mkanda wa usalama? Wakati fulani magari huendeshwa kwa kasi sana na kuishia kuanguka. Nyakati zingine utagundua kuwa madereva wengine huendesha magari wakiwa walevi chakari. Hili ni tendo la kipumbavu sana.

Pia, si jambo la ajabu kupata magari yakibeba abiria wengi kupita kiasi. Mara kwa mara, wale wanaovunja sheria za barabara hupeana hongo ili waendeleze tabia zao mbaya. Kila mmoja afuate sheria ili tupunguze ajali za barabarani.

31. Mwandishi anasema kuwa ni nini ambacho ni muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku?
    A. Pesa B. Chakula
    C. Usafiri D. Afya
32. Ni usafiri gani ambao hutumika sana?
    A. Hewani B. Angani
    C. Majini D. Barabarani
33. Magari ambayo si ya kibinafsi ni gani?
    A. Ya umma B. Ya watu
    C. Ya uma D. Ya umati
34. Ikiwa unataka kufika haraka sana, utatumia
    A. Ndege B. Piki piki
    C. Gari la kibinafsi D. Riksho
35. Ni nahau gani inayomaanisha wafariki?
    A. Wapige dua
    B. Wagonge mwamba
    C. Wakate kamba
    D. Wapige kamsa
36. Magari yanapoendeshwa kwa haraka na mwishowe kuanguka, tunaweza tukatumia methali gani?
    A. Ajali haina kinga
    B. Haraka haraka haina baraka
    C. Ajali haijali
    D. Kifo hakichagui
37. Hongo hupewa nani kulingana na kifungu hiki?
    A. Dereva B. Kondakta
    B. Abiria D. Polisi
38. Sababu kuu ya ajali za barabarani ni gani?
    A. Kutofuata sheria za barabarani
    B. Kutojali kwa wanaotumia barabara.
    C. Barabara mbovu
    D. Kuendesha magari kwa kasi
39. Ni tendo gani ambalo ni la kipumbavu kulingana na habari hii?
    A. Madereva kuendesha magari wakiwa walevi.
    B. Magari kuendeshwa kwa kasi
    C. Abiria kutofunga mishipi ya usalama
    D. Magari kubeba abiria wengi sana.
40. Ni nani anayefaa kufuata sheria ili tupunguze ajali?
    A. Abiria B. Dereva
    C. Sisi sote D. Polisi

**<u>Soma ushairi huu kisha ujibu maswali 41-50</u>**

Ukimwi ondoka hapa, unatutia mashaka,
Roho zetu zinapapa, jina lako kutamka,
Sote tunakuogopa, nani anayekutaka?
Ukimwi wacha kuua, tunayataka maisha.

Umeua babu yangu, nyanya baba hata mama,
Unawaua Wazungu, wahindi, Meka na Bana,
Wameliza ulimwengu, nyuyoki na Hiroshima,
Ukimwi wacha kuua, tunayataka maisha

Hakuna anakupenda, ila awe hayawani,
Mwenye bongo atashinda, ajichunge maishani,
Ama sivyo atakonda, hadi kule kaburini,
Ukimwi wacha kuua, tunayataka maisha.

Nyinyi msiokanyika, sasa leo nawambia,
Ugonjwa unatibika, na kifo hakina dawa,
Ukimwi ukikushika, kaburini utaingia,
Ukimwi wacha kuua, tunayataka maisha.

Siwezi kuishi pekee, upweke kweli uvundo,
Maoni yangu mshike, maunze badili mwendo,
Muache yenu makeke, fuata mema matendo,
Ukimwi wacha kuua, tunayataka maisha.

41. Shairi hili ni la aina gani?
    A. Tathlitha
    B. Tarbia
    C. Takhmisa
    D. Tathmia
42. Fafanua kibwagizo cha shairi hili.
    A. Ukimwi ondoka hapa, unatutia shaka
    B. Siwezi kuishi pekee, upweke ukweli uvundo.
    C. Ukimwi wacha kuua, tunayataka maisha
    D. Wamaliza ulimwengu. Nyuyoki na itiroshima.
43. Mshororo wa mwisho usiorudiwarudiwa huitwa?
    A. Kibwagizo
    B. Kiitikio
    C. Mkarara
    D. Kituo
44. Shairi hili lina beti ngapi?
    A. Nne B. Tano
    C. Tatu D. Sita
45. Kulingana na ubeti wa pili.
    A. Ukimwi ni kifo
    B. Ukimwi unaua wazungu pekee
    C. Ukimwi si tishio
    D. Ukimwi unabagua wakuua
46. Ugonjwa wa ukimwi
    A. Una tiba
    B. Hauna dawa
    C. Unaheshimu waliosoma
    D. Unawakandamiza wasiojiweza.
47. Mshororo wa kwanza katika ubeti wa pili una mizani mingapi?
    A. Kumi
    B. Kumi na mine
    C. Kumi na sita
    D. Minane
48. Onyesha kina cha kati cha mshororo wa tatu katika ubeti wa kwanza.
    A. ngu B. ni C.ma D.pa
49. Mtu anayetunga mashairi huitwaje?
    A. Malenga B. Manju
    C. Mjuzi D. Mwinyi
50. Toa kichwa mwafaka cha ushairi huu
    A. Kifo B. Mashaka
    C. Ukimwi D. Maisha duni